**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BUNGE LA TANZANIA**

*Simu:* +255 026 2322761-5
*Fax No.* +255 026 2324218
E-mail: cna@bunge.go.tz

Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro
S.L.P. 941,
40490 Tambukareli,
**DODOMA.**

**TAARIFA KWA UMMA**

Kamati nne (4) za Kudumu za Bunge zinawaalika wadau kutoa maoni kuhusu Miswada minne ya Sheria siku ya Jumatano tarehe 15 Januari 2025, kuanzia saa tatu kamili asubuhi, Ofisi ya Bunge, Jijini Dodoma. Kamati hizo na Miswada husika ni kama ifuatayo:-

Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria itapokea maoni ya wadau kuhusu **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.4) wa mwaka 2024** *[The Written Laws (Miscellaneous Ammendments) (No.4) Bill,2024]*, katika **Ukumbi wa Frank Mfundo**, uliopo ghorofa ya 5 katika jengo la Utawala.

Kamati ya Maji na Mazingira itapokea maoni ya wadau kuhusu **Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira wa mwaka 2024** *[The Enviromental Management (Ammendment) Bill, 2024]* katika **Ukumbi namba 41,** uliopo Jengo Dogo la Utawala (Utawala Annex).

Nayo, Kamati ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii itapokea maoni ya wadau kuhusu **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kazi wa mwaka 2024** *[The Labour Laws (Ammendments) Bill, 202],* katika **Ukumbi wa Msekwa Lounge**, Jengo la Pius Msekwa.

Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) itapokea maoni ya wadau kuhusu **Muswada wa Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi wa mwaka 2024,** katika **Ukumbi namba 20,** Jengo Dogo la Utawala (Utawala Annex).
Wadau wote wenye maoni kuhusu Miswada hiyo wanaalikwa kufika na kuwasilisha maoni yao kwenye Kamati husika.

Aidha, maoni yanaweza pia kutumwa kwa njia ya Posta kupitia anuani ya Ofisi ya Bunge au kupitia Barua pepe ya *cna@bunge.go.tz* au *kamati@bunge.go.tz*. Miswada hiyo inapatikana katika tovuti ya Bunge ya www.bunge.go.tz .

**Imetolewa na:** Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma,
Ofisi ya Bunge,
**DODOMA.**

09 Januari 2025.